



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA



WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

TAARIFA KWA UMMA

MATUMIZI YA MFUMO ULIOBORESHWA WA UTOAJI HUDUMA

Dar es Salaam – 08 Aprili, 2026

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) katika kufanya maboresho na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma, inapenda kuwataarifu wadau wote na umma kwa ujumla kuhusu kuanza kutumika kwa mfumo ulioboreshwa wa utoaji huduma unaofahamika kama BRELA Online Services (BOS) kuanzia tarehe 08 Aprili, 2026.

Mfumo wa BOS umeanza kutoa huduma ya usajili wa maombi mapya ya majina ya biashara na leseni za viwanda. Hivyo, wadau wanaokusudia kuwasilisha maombi mapya ya huduma tajwa kuanzia sasa wanapaswa kutumia kiunganishi <https://bos.brela.go.tz>.

Kwa mteja mwenye maombi yanayoendelea, atakamilisha maombi yake kwenye mfumo wa zamani wa ORS wenye kiunganishi <https://ors.brela.go.tz>.

Aidha, kwa mteja mwenye akaunti ya ORS, ili kuingia kwenye akaunti ya BOS atapaswa kutumia njia mojawapo kati ya hizi; mosi, atapaswa kuingiza anuani ya baruapepe aliyotumia kufungulia akaunti katika mfumo wa awali na kubonyeza kitufe cha 'forget password,' kisha atapokea baruapepe itakayomwezesha kuingia kwenye mfumo wa BOS. Pili, anaweza kutengeneza account mpya kupitia kitufe cha "create new account" ambapo atapokea baruapepe itakayomwezesha kuingia kwenye mfumo wa BOS.

Huduma zilizobaki; usajili wa kampuni, hataza, alama za huduma na biashara, pamoja na maombi yanayoendelea zitaendelea kutolewa kupitia mfumo wa ORS.

Kwa usaidizi wa haraka, tafadhali wasiliana nasi kupitia namba ya simu +255 (0) 22 2212800 au andika kupitia baruapepe support.bos@brela.go.tz

Imetolewa na;

Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma